JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

TAARIFA YA WILAYA YA SERENGETI KWA

MHE. KASSIM MAJALIWA MAJALIWA (MB) WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA TAREHE 18.01.2018

Imeandaliwa na

Ofisi ya Mkuu Wilaya,
P. O. Box, 20,
MUGUMU / SERENGETI.
Simu Na. 0732 - 985962
Fax Na. 0732 - 985962
E-mail: das.serengeti@mara.go.tz

18 Januari, 2018

TAARIFA YA MAENDELEO YA WILAYA YA SERENGETI KWA MHE. KASSIM MAJALIWA MAJALIWA (MB), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA TAREHE 18/01/2018

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Awali ya yote ninapenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kukufikisha salama katika Wilaya yetu ya Serengeti. Pia kwa niaba ya Wananchi wa Wilaya ya Serengeti ninapenda kukukaribisha wewe na msafara wako Wilayani kwetu.

Aidha, napenda kuchukua fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Dr. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuthibitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kura zote kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sisi Wananchi wa Serengeti tunakupongeza kwa kazi nzuri unayoifanya ya kuwatumikia Watanzania, na tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu akubariki katika majukumu yako.

Mipaka ya Wilaya

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ya Serengeti ni mojawapo ya Wilaya sita (6) zinazounda Mkoa wa Mara. Wilaya ya Serengeti kwa upande wa Kaskazini imepakana na Nchi ya Kenya, upande wa Mashariki inapakana na Wilaya ya Ngorongoro (Mkoa wa Arusha), Kusini imepakana na Wilaya ya Bunda na Bariadi (Mkoa wa Simiyu), Magharibi imepakana na Wilaya ya Butiama na Kaskazini Magharibi imepakana na Wilaya ya Tarime.

Eneo la Utawala na idadi ya watu

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ya Serengeti inaundwa na Tarafa nne (4) Kata (30), Vijiji 78 na Vitongoji 363 vikiwemo vitongoji 23 vya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mugumu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ina ukubwa wa kilometa za mraba 10,373, kati ya eneo hilo kilometa za mraba karibu 7,000 ni Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Aidha kilometa za mraba 558.9 ni eneo la Pori la Akiba la Ikorongo, Kilometa za mraba 434.5 ni eneo la Pori la Akiba Gurumeti na kilometa za mraba 242.3 ni eneo la Taasisi ya Kijamii ya Uhifadhi wa Wanyamapori - WMA. Eneo lililobaki la kilometa za mraba 2,137.3 ni eneo la Makazi, kilimo, ufugaji na matumizi mengine.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, Wilaya ilikuwa na jumla ya Wakazi 249,420 kati yao (Wanaume ni 121,399 na Wanawake 128,021) ikiwa na jumla ya kaya 41,570. Ongezeko la watu kwa mwaka ni wastani wa asilimia 2.8. Kwa sasa Wilaya inakadiriwa kuwa na jumla ya wakazi wapatao 294,367 kati yao (Wanaume 143,275 na Wanawake 151,091) na kaya zipatazo 49,060.

Ulinzi na Usalama

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Hali ya usalama wa wananchi na mali zao imeendelea vizuri, hakuna matukio makubwa ya uvunjifu wa amani. Matukio yaliyopo ni madogo madogo kama vile ugomvi unaosababisha watu kujeruhiana na matukio machache ya wizi

wa mifugo hasa maeneo ya Borenga (Serengeti) na Mrito (Tarime), na makosa ya ukatili wa kijinsia. Hata hivyo matukio hayo yamekuwa yakidhibitiwa na vyombo vya Ulinzi na Usalama, ngazi za uongozi za Kata na Vijiji hivyo kufanya hali kuwa shwari

Hali ya Kisiasa

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ya Serengeti ina Jimbo moja la Uchaguzi ambalo ni Jimbo la Serengeti. Katika uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 25/10/2015, Chama cha Mapinduzi kilishinda viti 12 vya udiwani na CHADEMA kilishinda viti 18. Madiwani wa viti maalum wapo 11, kati yao wanne ni kupitia Chama cha Mapinduzi na 7 ni kupitia CHADEMA, Kwa hiyo Wilaya ina jumla ya Madiwani 41. Aidha, Mbunge wa Jimbo la Serengeti Mhe. Marwa Ryoba Chacha alichaguliwa kupitia chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na Mbunge wa viti maalum Mhe. Catherine Nyakaho Ruge kupitia chama hicho.

Hali ya Uchumi

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Uchumi wa Wilaya ya Serengeti kwa sehemu kubwa unategemea Kilimo, ufugaji na Utalii. Sekta hizi huchangia 85% ya pato la Wilaya. Wakazi wachache hujishughulisha na biashara ndogondogo kama vile maduka, ufugaji wa nyuki, migahawa, mashine za kusaga, useremala, uchimbaji wa madini na usindikaji mazao. Wastani wa pato la mwananchi kwa mwaka 2015/2016 ni Tshs 1,572,899/=.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ya Serengeti ina jumla ya Viwanda vidogo vinne (4) na viwanda viwili (2) vipo kwenye hatua ya ujenzi. Ujenzi wa viwanda hivyo utakapokamilia utafanya Wilaya kuwa na jumla ya viwanda sita (6). Viwanda hivi vinatarajiwa kutoa ajira kwa wakazi wa Wilaya ya Serengeti na kuongeza mapato kwa Serikali.

Wilaya ina jumla ya Benki 2 ambazo ni **National Microfinance Bank-NMB**, na **CRDB** vilevile kuna Taasisi zingine za fedha ambazo ni **BAYPORT, Benki za Kijamii (VICOBA) na SACCOS** ambazo pia zinatoa huduma za kifedha na mikopo kwa wananchi.

SEKTA YA KILIMO

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kwa kipindi cha mwaka 2015/2016 na 2016/2017 uzalishaji wa mazao ya chakula Wilayani umekuwa ukipanda na kushuka kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa. Jumla ya tani 169,028 za chakula zilizalishwa katika msimu wa mwaka 2015/16, ulikinganisha na tani 101,074 za chakula mwaka 2016/17. Mabadiliko haya ya uzalishaji wa mazao umetokana na ukame na visumbufu vya mimea.

Kilimo cha Zao la Pamba

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ya Serengeti ni mojawapo ya Wilaya zinazolima zao la Pamba mkoani Mara. Katika msimu wa Kilimo 2016/17 Wilaya ililenga kulima ekari 28,500, hata hivyo jumla ya ekari 10,637.5 tu ndio zililimwa. Matarajio ya uzalishaji kwa ekari katika Wilaya yalikuwa ni 450 – 750. Uzalishaji wa zao la Pamba ulikuwa jumla ya kilogramu 2,029,140, ambapo uzalishaji halisi ulikuwa wastani wa kilogramu 191 kwa ekari.

Katika msimu wa Kilimo 2017/18, Wilaya umewahamasisha wakulima ili kulima zao la Pamba, ambapo jumla ya wakulima 8,269 wamesajiliwa na wamelima jumla ya ekari 21,208. Kutokana na ekari 21,208 zilizolimwa mpaka mwezi Desemba, 2017, matarajio ya mavuno ni kilogramu 12,724,800, hata hivyo shughuli za upandaji bado zinaendelea hadi Janaury 15, 2018. Hivyo tunatarajia jumla ya ekari zitakazopandwa zitaongezeka na kilo zinazotarajiwa kuvunwa zitaongezeka.

MKAKATI WA WILAYA KUINUA UZALISHAJI WA PAMBA

Lengo la Wilaya ni kuongeza tija kutoka wastani wa kilo 550 kwa ekari hadi 1000 ifikapo 2020 kwa kutekeleza yafuatayo:-

- Matumizi sahihi ya Mbegu bora aina ya UK M08 na Viuatilifu vya Pamba.
- Kutumia vikosi kazi vilivyopo katika ngazi za Vijiji, Kata na Wilaya katika kusimamia shughuli za Kilimo cha Pamba.
- Kusajili wakulima wa Pamba katika Rejista za Vijiji na kusimamia matumizi yake, ambapo jumla ya Wakulima 8,269 tayari wamesajiliwa.
- Kuanzisha mashamba ya mfano ya Pamba 2 kwa kila Kijiji, ambayo yatatumika kufundishia wakulima kanuni mbalimbali za kilimo bora cha Pamba.
- Kuboresha kwa mbinu za uhamasishaji na ufikishaji wa mbinu za elimu ya kilimo bora cha pamba kwa kuwashirikisha wakulima wawezeshaji, na kuongezeka kwa uzalishaji na ubora wa pamba.
- Kuimarika kwa mfumo wa soko la pamba nchini, hasa bei ya pamba kwa wakulima kutoka wastani wa Tshs. 440 hadi 1,000 kwa kilo kwa sasa.
- Kuanzisha mfumo mzuri na imara wa uzalishaji mbegu bora za pamba na kuzisambaza kwa wakulima.

KUENDELEZA KILIMO CHA UMWAGILIAJI

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ya Serengeti inakadiriwa kuwa na eneo la hekta 6,083 linalofaa kwa Kilimo cha Umwagiliaji. Hata hivyo, kati ya hizo hekta 957 tu ndizo hutumika kwa ajili ya kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji Wilayani, ambavyo hekta 853 humwagiliwa kwa njia ya asili na hekta 104 umwagiliaji wa kutumia mifereji iliyojengwa katika Skimu ya Nyamitita na Bugerera.

SEKTA YA USHIRIKA

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ina jumla ya vyama vya ushirika vya msingi 69 vilivyoandikishwa kwa mujibu wa sheria ambavyo vyama hivyo vimegawanyika kama ifuatavyo; vyama vya mazao ni 12, SACCOs 41, Mifugo 5, ukamuaji mafuta 1, mapishi na mapambo 1, utumiaji umeme wa upepo 1 na vyama vya walaji (consumers) 2 na madini 3. Pia kuna vyama vya awali vya ushirika vya zao la pamba 83.

Hadi kufikia Juni 2017, vyama vya ushirika vya msingi vilikuwa na wanachama wapatao 4107 (wanaume 2654, wanawake 1453). Hisa na akiba katika vyama hivi ni Tshs.851,810,000.00, mikopo iliyotolewa ni Tshs. 506,186,000 na mikopo iliyorejeshwa ni Tshs. 4,817,913,000, hivyo mikopo isiyorejeshwa ni Tshs. 1989,470,000.

Ili kuboresha vyama vya ushirika vya msingi hasa SACCOs ziwe endelevu Wilaya ina mikakati ifuatayo:-

- Kuwahamasisha wananchi kuunda vyama vya ushirika kwa kushirikiana na wadau wengine wa ushirika.
- Kutoa elimu ya ushirika kwa wanachama, viongozi na Watendaji wa vyama vya ushirika juu uya usimamizi na uendeshaji wa vyama hivyo.

SEKTA YA MIFUGO

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ya Serengeti imeendelea kusimamia shughuli mbalimbali za uendelezaji wa mifugo ambazo ni ushauri kwa wafugaji, ukaguzi wa nyama, utengaji wa malisho kupitia mipango ya matumizi bora ya ardhi, tiba na kinga ya magonjwa mbalimbali na biashara ya mifugo. Mtindo wa ufugaji unaotumika, ni ufugaji huria(*extensive system*).

Uboreshaji wa Mifugo ya Asili

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Uongozi wa Wilaya kwa kushirikiana na sekta binafsi imeendelea kuiboresha Mifugo ya Asili kwa njia ya Uhimilishaji (Artificial Insermination). Lengo ikiwa ni kuongeza tija katika uzalishaji wa maziwa na nyama ili kumwezesha mfugaji kupata kipato kizuri.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Jumla ya ng'ombe 640 walipandishwa kwa chupa ambapo ndama 582 walizaliwa. Aidha, hadi sasa kuna Wafugaji 25 wenye madume bora ambapo 54 walisambazwa Wilayani na madume 65 wamenunuliwa na Wafugaji baada ya kupata elimu ya kuboresha mifugo yao.

KINGA NA TIBA

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ya Serengeti imeendelea kuchukua hatua kupambana na magonjwa ya mifugo ambayo ni pamoja na yale yaenezwayo na kupe (Tick borne Diseases), Minyoo na Mdondo (NCD).

MCHANGO WA SEKTA YA MIFUGO KWA UCHUMI WA MWANANCHI

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ina jumla ya minada 13 inayouza mifugo na kusafirishwa sehemu mbalimbali. Idadi ya mifugo hai iliyouzwa na kusafirishwa nje ya Wilaya imeongezeka kutoka 53,796 kwa mwaka 2015/2016 hadi 71,929 mwaka 2016/2017. Aidha, uzalishaji wa mazao mengine ya mifugo, hususani maziwa, nyama na mayai umeongezeka na kuwaongozea wananchi kipato.

UPIGAJI CHAPA NA USAJILI WA MIFUGO

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ya Serengeti ilizindua kampeni ya kupiga chapa ng'ombe na kusajili wafugaji na mifugo mwezi Oktoba, 2017. Lengo la Wilaya ni kupiga chapa na kusajili ng'ombe 385,542, mbuzi 151,531 kondoo 99,035, nguruwe 702, kuku 269,444 na mbwa 24,219. Kazi hii inaendelea katika kata zote 30 zenye jumla ya vijiji 78.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Hadi sasa kazi hii imeshakamilika katika vijiji 30, ambapo jumla ya ng'ombe 163,261 (42%), mbuzi 62,829 (41), Kondoo 97,355 (98), nguruwe 208

(30), na Punda 1,031 wamesajiliwa na kupigwa chapa. Zoezi la usajili na kupiga chapa mifugo linaendelea. Pamoja na mafanikio hayo kumekuwepo na changamoto mbalimbali, kama vile wahamiaji toka Wilaya ya jirani, viongozi wa kisiasa kuingilia zoezi hasa katika vijiji vya Nyamakobiti, Iserere na Magatini. Hata hivyo uongozi wa Wilaya kwa kushirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama imeendelea kusimamia utekelezaji wake.

SEKTA YA ARDHI

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya imeendelea kupima viwanja vya makazi, biashara na matumizi mengine ili kupunguza na kuondoa makazi holela katika mji wa Mugumu na miji midogo midogo ya pembezoni inayokua kwa kasi.

Hadi kufikia Desemba, 2017, jumla ya viwanja 4,392 vimepimwa na kumilikishwa kwa wananchi. Viwanja hivyo vimepimwa katika maeneo ya Mji Mdogo wa Mugumu, jumla ya Michoro 2 imeendaliwa kwa ajili ya mji mdogo wa kibiashara wa Natta Mbisso unaokua kwa kasi. Aidha, Wilaya inaendelea kutenga fedha kila mwaka ili kuhakikisha kuwa wananchi wanaishi katika maeneo yaliyopangwa vizuri.

Mpango wa matumizi bora ya Ardhi

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Hadi kufika Desemba 2017, jumla ya Vijiji 10 vimetekeleza mpango wa Matumizi bora ya Ardhi na jumla ya Hati Milki za Kimila 700 zimeandaliwa kati ya hizo hati 330 za Kimila zimetolewa kwa wananchi, na hati 370 bado hazijatolewa kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo baadhi ya Wananchi kuuza sehemu za mashamba hayo bila kufuata utaratibu hivyo kukosa sifa za kusajili na kutolewa kwa hati hizo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi katika Wilaya ya Serengeti ulizinduliwa rasmi na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. William Lukuvi (Mb) tarehe 29/11/2017. Mpango huo umelenga kupanga ardhi, kutatua migogoro ya ardhi, kupunguza mwingiliano wa matumizi ya ardhi kati ya binadamu na wanyamapori, kuhamasisha uhifadhi endelevu, kuboresha matumizi ya rasilimali, kudhibiti kuhamahama kwa watu hasa wafugaji na kusaidia kuhifadhi maeneo muhimu na vyanzo vya maji pamoja na kutenga maeneo ya uwekezaji katika sekta za Usafiri na Usafirishaji, Viwanda na Utalii.

MIGOGORO YA ARDHI

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya imeendelea kutatua migogoro ya ardhi kwa kuzingatia Sheria na taratibu zilizopo. Mabaraza ya Kata yamekuwa yakitumika katika kutatua migogoro ya ardhi. Wananchi wasioridhika na utatuzi wa migogoro katika ngazi hiyo wamekuwa na fursa ya kukata rufaa katika mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya ili kupata haki zao.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Tunalo tatizo la migogoro ya mipaka kati ya Vijiji vinavyozunguka Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na Hifadhi. Mgogoro huo unashughulikiwa na Mamlaka husika. Aidha, upo mgogoro wa mpaka kati ya Wilaya ya Serengeti, Butiama na Bunda katika eneo la Remung'orori na

Mikomariro. Mgogoro huo ni wa siku nyinyi na ulishawahi kutafutiwa ufumbuzi na Viongozi wa Mkoa na Wilaya waliopita. Lakini mgogoro huo umekuwa ukijirudia mara kwa mara. Kwa sasa suala hili Mhe. Mkuu wa Mkoa analishughulikia.

UHIFADHI WA MAZINGIRA.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira, uongozi wa Wilaya umeendelea kusimamia shughuli za uhifadhi ikiwa ni pamoja na kutoa Elimu ya Uhifadhi kwa wananchi. Kuanzia mwaka 2009 hadi 2016, jumla ya wanafunzi 2,000 wamepatiwa mafunzo ya hifadhi ya mazingira katika kituo cha elimu ya Mazingira (Environmental Education Center) ili kusaidia vijana wanaomaliza masomo ya Sekondari kuwa mabalozi wazuri wa kuhifadhi mazingira katika maeneo yao.

UPANDAJI MITI

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Katika mwaka 2016/2017 na 2017/2018 Wilaya imweza kupanda jumla ya miche ya miti 1,092,216 ambayo ni sawa na asilimia 73 ya lengo liliokusudiwa la kupanda miti 1,500,000. Wilaya imejiwekea mikaakati mbalimbali ili kuhakikisha kuwa kufikia Desemba 2018 imefikia lengo la kuwa na miti 1,500,000.

UKUSANYAJI NA USIMAMIZI WA MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Halmashauri imeweza kuimarisha ukusanyaji na usimamizi wa mapato, ambapo katika mwaka wa fedha 2015/2016 tulikusanya jumla ya Tshs 3,298, 258,500.65 sawa na asilimia 95 ya makisio ya mapato kwa mwaka husika. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri iliweza kukusanya jumla Tshs 3, 185, 535,982.96 ambayo ni sawa na asilimia 97 ya mapato kwa mwaka.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kushuka kwa mahitaji ya wanunuzi wa zao la Tumbaku Wilayani kumechangia kushuka kwa mapato ya Halmashauri, kwani katika mwaka wa fedha 2015/2016 mapato yanayotokana na zao la Tumbaku yalikuwa Tshs 810, 000,000 na mwaka wa fedha 2016/2017 mapato hayo yameshuka hadi kiasi cha Tshs 366, 989,000 sawa na pungufu ya aslimia 55.

Hata hivyo, Halmashauri inaendelea kufuatilia na kusimamia ukusanyaji wa mapato katika vyanzo vingine ili kuziba pengo hilo na kupunguza utegemezi wa Ruzuku toka Serikali Kuu.

FEDHA ZA MAENDELEO KUTOKA SERIKALI KUU

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Katika mwaka wa fedha 2017/2018 halmashauri iliidhinishiwa kutumia kiasi cha **Tshs 6,609,778,720.94** kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya Maendeleo kutoka Serikali Kuu. Hadi kufikia Desemba 2017, halmashauri imepokea jumla ya shilingi **1,126,653,030** sawa na asilimia 17 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta za Huduma za Jamii na Kiuchumi.

UWEZESHAJI WA WANANCHI KIUCHUMI

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Katika kueneza dhana ya Maendeleo ya Jamii kwa wananchi (kazi za kujitegemea) Wilaya imeendelea kuwawezesha wananchi kuanzisha Benki za Jamii Vijijini (VICOBA) na kuzisimamia wenyewe. Kwa kipindi cha 2014/15 hadi 2016/17 wanachama katika vikundi 74 vya VICOBA wameweza kujiwekea akiba ya Tsh **1,371,547,150.00**

MIKOPO YA WANAWAKE NA VIJANA

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Katika kipindi cha kuanzi mwaka 2014/2015 hadi 2016/2017, kupitia mfuko wa Wanawake na Vijana, Halmashauri ya Wilaya imetoa mikopo na mafunzo ya kujenga uwezo kwa vikundi 55 vya Vijana na vikundi 73 vya Wanawake yenye thamani ya Tshs **367,500,000;** na hivyo katika Mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri imetoa mikopo ya Vijana na Wanawake yenye thamani ya Tshs **103,000,000/-** kwa vikundi vya wanawake na vijana.

UTEKELEZAJI WA MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII-TASAF

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Utekelezaji wa Mpango wa TASAF III Wilayani Serengeti ulianza rasmi mwezi Julai, 2014 ambapo ulihusisha Vijiji 57 vilivyofanikiwa kuingia katika mpango. Mpaka sasa malipo kwa Walengwa yamefanyika kwa awamu kumi na tatu (13) kuanzia Julai, 2015 hadi Disemba, 2017. Jumla ya Fedha zote zilizopokelewa ni Tshs. 2,216,639,492.90, Fedha zilizotumika kuwalipa walengwa ni Tshs. 1,445,904,000 na Fedha zilizorejeshwa TASAF makao makuu ni Tshs. 37,000,000 kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo vifo, kuhama na kukosa sifa. Kiasi kilichobaki ni fedha za uendeshaji wa ofisi, ufuatiliaji ngazi ya wilaya na vijiji.

SEKTA ZA HUDUMA ZA JAMII

Sekta ya Afya

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ina Hospitali 1 inayomilikiwa na Kanisa la Mennonite Tanzania, Vituo vya Afya 7, Zahanati 46. Aidha, Vijiji 54 kati ya 78 vina Vituo vya kutolea huduma za afya sawa na asilimia 69.

UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Katika kutekeleza agizo la Serikali la kila Halmashauri kujenga hospitali za Wilaya ili kupunguza msongamano katika hospitali za Mikoa, Wilaya inaendelea na Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, ambapo kwa ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD) upo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Pia jengo la upasuaji limekamilika likiwa na vifaa vyote vinavyotakiwa.

WATUMISHI KATIKA SEKTA YA AFYA

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ina watumishi wa Afya 403 kati ya hao (84 ni waajiriwa wa Kanisa la Mennonite Tanzania) Mahitaji halisi ya Watumishi katika Sekta ya Afya ni 1,014 hivyo kuna upungufu wa watumishi 611 sawa na 60.3%

Hata hivyo Idara imepokea Watumishi 10 wa (Kada mbalimbali za Afya) na Wasaidizi wa Mahesabu 5 katika mwaka huu wa fedha wa 2017/2018. Pamoja na upungufu huu wa Watumishi, kwa sasa vituo vyote vya kutolea huduma za afya vina angalau Watumishi wawili wenye sifa kwa kila Kituo ili kuhakikisha Wananchi wanapata huduma stahiki.

Udhibiti wa maambukizi ya UKIMWI

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya imeendelea na jitihada zake katika udhibiti maambukizi mapya ya UKIMWI ikiwa ni pamoja na kutoa dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI (ARVs). Katika kipindi cha Julai – Desemba2017 jumla ya watu 987 (Wanaume 477 na Wanawake 510) walipima afya zao na kati yao 45 (Wanaume 16 na Wanawake 29) walibainika kuwa na maambukizi ya UKIMWI. Kiwango cha maambukizi kwa Wilaya ni 4%.

Utoaji wa Huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ina jumla ya vituo 47 vinavyotoa huduma za Afya ya uzazi na Mtoto (RCH) ikiwa ni pamoja na hospitali ya Nyerere DDH.

Idadi ya akina mama wajawazito wanaohudhuria kliniki na kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma za Afya imekuwa ikiongezeka na pia vifo vya wajawazito vimekuwa vikipungua kutoka 40/100,000 kwa mwaka 2015 hadi 32/100,000 kwa mwaka 2017. Kuongezeka kwa mahudhurio na kujifungulia kwa wajawazito katika vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na kupungua kwa vifo vya wajawazito vimesababishwa na kuanzishwa kwa huduma za upasuaji (*CEmONC services)* katika Kituo cha Afya Natta na Iramba.

Vifo vya Watoto Wachanga

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Vifo vya watoto wachanga vinapungua kutoka vifo 7/1,000 kwa mwaka 2015 hadi vifo 3/1,000 kila uzazi kwa mwaka 2017, hii ni kutokana na mikakati ya kuhimiza wajawazito kuhudhuria kliniki na kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma za Afya.

Huduma za Upasuaji

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ina vituo vitatu (3) vinavyotoa huduma za upasuaji wa dharura kwa wajawazito (CEmONC services) ambavyo ni Hospitali ya Nyerere DDH na Vituo vya Afya Natta na Iramba. Aidha, mwezi Desemba 2017, Wilaya imepokea jumla ya Tshs 400,000,000/= ikiwa ni kwa ajili ya Uboreshaji wa Miundombinu katika Kituo cha Afya cha Natta. Mpango wa Serikali ni kuboresha huduma za Afya katika Vituo vya Afya vya Natta na Iramba.

Chanjo kwa watoto chini ya miaka 5

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Katika kukabiliana na tatizo la vifo vya watoto wachanga walio chini ya umri wa miaka mitano, Uongozi wa Wilaya umejiwekea mkakati wa kuhakikisha kwamba watoto wanaostahili kupata chanjo wanapata chanjo ili kujikinga na magonjwa yanayozuilika kwa chanjo. Idadi ya watoto chini ya mwaka mmoja waliopata chanjo imeongezeka kutoka watoto 10,678 kwa mwaka 2016 hadi watoto 11,452 zaidi ya watoto 10,716 waliotegemewa kwa Mwaka 2017 sawa na ongezeko la watoto 736.

Dawa na Vifaa tiba katika vituo vya huduma za Afya

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Hali ya upatikanaji wa dawa katika vituo vya kutolea huduma kwa sasa ni asilimia 87% na kwa sasa vituo vinaagiza na kupokea dawa na vifaa tiba kutoka katika bohari kuu ya dawa kanda ya ziwa (MSD Mwanza) kulingana na mahitaji.

Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Idadi ya wanachama waliojunga na Mfuko wa Afya ya Jamii toka kaya 10,306 kwa mwaka 2016 ambayo ilikuwa sawa na asilimia 21 hadi kufikia Desemba 2017 imeongezeka na kufikia kaya 11,744 kati ya Kaya 49,060 zinazotegemewa ambayo ni sawa na asilimia 27.4. Wilaya inaendelea na jitihada za kuhamasisha jamii kupitia vikao na mikutano mbalimbali kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) ili kufikia lengo la Mkoa asilimia 30 ya kaya zinazotakiwa kujiunga.

Matibabu ya Wazee

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ya Serengeti imeendelea kutoa huduma za Afya kwa wazee katika vituo vyake vya kutolea huduma kwa mujibu wa Sera na Miongozo ya Serikali. Jumla wazee **11,946** wametambuliwa kati yao 9000 ndiyo waliokidhi vigezo vya kupata matibabu bure. Aidha, jumla ya Wazee **8,800** wameshapewa vitambulisho vyao vya matibabu. Pia zoezi la kuwapiga picha Wazee 200 waliobaki linaendelea kwa wale ambao hawakupata nafasi ya kupigwa picha. Hata hivyo katika kuboresha huduma za Afya katika kundi la wazee Halmashauri imenunua mashine ya kisasa ya kutengeneza vitambulisho vya Wazee wote na leo utatuzindulia mpango huo.

Ujenzi wa vituo vya kutolea Huduma za Afya;

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ya Serengeti inaendelea kusogeza huduma za Afya kwa wananchi waweze kupata huduma za Afya kwa umbali usiozidi kilomita 5 kama ilivyo Sera ya Taifa ya Afya, na kila kijiji kuwa na zahanati na kata kuwa na kituo cha Afya.

Katika kutekeleza maelekezo hayo ya Serikali, Wilaya ya Serengeti imeendelea na ujenzi wa Zahanati katika Vijiji ambavyo havina zahanati na zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Hadi sasa ujenzi wa zahanati unaendelea katika vijiji vya Magange, Motukeri, Kegonga, Nyirongo, Somoche, Busawe, Kenokwe, Burunga na Koreli ambao upo katika hatua mbalimbali.

SEKTA YA ELIMU

Elimu ya Awali

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ya Serengeti ina jumla ya Shule za awali 115 kati ya hizo za serikali zikiwa 111. Hadi kufikia Machi, 31, 2017 jumla ya watoto 12,003 wenye umri wa miaka 4 na 5 wameandikishwa, kati yao wavulana 6,448 na wasichana 5,555 katika shule za awali. Hata hivyo watoto wote wa shule za awali katika Wilaya wanatumia madarasa yaliyopo katika shule za msingi.

ELIMU YA MSINGI

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ya Serengeti ina jumla ya Shule za msingi 115 ambapo shule za serikali ni 111 na za binafsi ni 4. Wilaya ina jumla ya wanafunzi **85,964** kati yao **84,682(**Wav **43,934** na Was **40,748)** sawa na asilimia 98.5 wapo katika shule za Serikali, na **1,282** (Wav **688** na Was **594)** sawa na asilimia 1.5 wanasoma katika shule za binafsi.

Uandikishaji

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ya Serengeti katika mwaka 2017, imeandiksha jumla ya wanafunzi 17,952 wa darasa la I wenye umri wa miaka 6 - 10 kati yao (wav 9,375 na Was 8,577) sawa na asilimia 133% ya lengo lililotarajiwa kuandikishwa la watoto 13,504. Aidha, wanafunzi wa Awali maoteo yalikuwa ni kuandikisha wanafunzi **13,212**, hata hivyo jumla ya wanafunzi **12,003** waliandikishwa sawa na asilimia **91.**

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ina jumla ya walimu 1,135 katika Shule za msingi 115 za Serikali. Pia, Wilaya imeendelea kuwa na upungufu wa walimu 966 kutokana na mwitikio mzuri wa wazazi katika suala zima la uandikishaji wa watoto katika shule za awali na msingi.

Madawati

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Hali ya madawati katika Wilaya Serengeti hadi kufikia Mwezi Oktoba **2017,** ina mahitaji ya madawati **28,227** katika Shule za Msingi yaliyopo ni **26,455** na hivyo kuwa na upungufu wa madawati **1,772.**

MIUNDOMBINU

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya imeendelea kuimarisha miundombinu ya Shule za Msingi ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa miundombinu katika shule. Dhamira ya Wilaya ni kuhakikisha kuwa mazingira ya kufundishia na kujifunzia yanakuwa rafiki kwa walimu na wanafunzi. Hadi kufikia mwezi Desemba 2014, halmashauri ina jumla vyumba vya madarasa 839, nyumba za walimu 565, matundu ya vyoo 1143 katika shule za msingi.

Ufaulu wa mtihani wa Taifa wa darasa la VII

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Hali ya Ufaulu katika Wilaya ya Serengeti ni nzuri ambapo kwa mwaka 2017 jumla ya wanafunzi **4,891** kati ya **6,196** sawa na asilimia 78.5 waliofanya mtihani wamefaulu kujiunga na Elimu ya Sekondari na kuifanya Wilaya kuwa ya kwanza Mkoa.

Hali ya mimba mashuleni

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Uongozi wa Wilaya ya Serengeti uemendelea kupamabana na changamoto ya mimba kwa wanafunzi wa shule za msingi kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama. Kuanzia mwaka 2015 hadi kufikia Desemba, 2017 jumla ya wanafunzi 30 katika shule za msingi waliacha masomo kwa tatizo la mimba. Hata hivyo, kwa mwaka 2016 jumla ya watuhumiwa 20 wamefikishwa polisi na majalada yamefunguliwa na upelelezi unaendelea. Aidha, kwa mwaka 2017, jumla watuhumiwa 3 wamefikishwa polisi na kufunguliwa majalada na upelelezi unaendelea, watuhumiwa 5 bado wanatafutwa na polisi, na 2 majadalada hayajafunguliwa.

Elimu ya Sekondari

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ya Serengeti ina jumla ya Shule za Sekondari **26,** shule **22** zinamilikiwa na Serikali, shule **04** zinamilikiwa na watu binafsi. Shule **20** za Serikali na **04** zisizo za serikali zina wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne na shule **02** za Serikali zina mikondo ya kidato cha Tano na Sita.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ya Serengeti ina jumla ya wanafunzi wapatao **9,742** kati yao wavulana ni **5,182** na wasichana ni **4,560.** Shule za serikali zina jumla ya wanafunzi 8,885 ikiwa wavulana 4,697 na wasichana 4,188, shule za binafsi zina jumla ya wanafunzi 857 ambao wavulana ni 485 na wasichana ni 372.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ya Serengeti ina jumla ya Walimu **459** wa Shule za sekondari za Serikali kati yao Walimu wa masomo ya **Sayansi na Hisabati 91 na** Walimu wa masomo ya Sanaa 368. Idadi ya walimu wa shule za Sekondari imeendelea kuongezeka kila mwaka, hata hivyo Wilaya bado ina upungufu mkubwa wa walimu 100 wa masomo ya Sayansi na Hisabati.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ya Serengeti imeendelea kuimarisha miundombinu ya Shule za Sekondari kulingana na mahitaji mbalimbali kwa kushirikiana na wananchi. Hata hivyo, mahitaji ya yameengozeka kutokana na ongezeko la wanafunzi waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka 2017 ambao ni 3,844 ukilinganisha na wanafunzi waliomaliza kidato IV mwaka 2016 ambao walikuwa jumla ya wanafunzi 1,893.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Katika kukabiliana na changamoto ya upungufu wa miundombinu katika shule za Sekondari Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti kwa kushirikiana na wananchi hadi kufikia mwezi Desemba, 2017 inaendelea na ukamilishaji ujenzi wa vyumba vya madarasa na kuhamasisha ukamilishaji wa jengo la Utawala katika Shule mpya ya Nyakitono Sekondari ukamilishaji wa ujenzi wa shule za Sekondari katika kata za Mosongo, Majimoto na Sedeco ili shule hizi ziweze kukamilika na kufunguliwa

Ujenzi wa Vyumba vya Maabara

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti inaendelea kukamilisha ujenzi wa vyumba vya maabara za Shule za Sekondari kwa kadri ya upatikanaji wa fedha toka Serikali Kuu lakini pia kwa kushirikiana kiasi kikubwa na wananchi.

Mapokezi ya Fedha za Elimu Msingi bila Malipo

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ya Serengeti imeendelea kupokea fedha toka Serikali kuu kwa ajili ya fidia ya ada, ruzuku (capitation grants) na shule za bweni hupokea pia fedha kwa ajili ya kugharamia chakula cha wanafunzi umeme na maji.

Malipo ya Madeni ya Watumishi (Walimu)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Katika kipindi cha Julai 2014 hadi Desemba, 2017 jumla Tshs 50,904,591 zimelipwa kwa walimu 68 ikiwa ni madeni yasiyo ya mishahara.

Maandalizi ya kupokea kidato cha I, 2018

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Katika Wilaya ya Serengeti idadi ya wanafunzi wanaojiunga na shule za Sekondari inaongezeka kila mwaka na hasa baada ya Serikali kuanza kutekeleza Mpango wa Elimu bila malipo mwaka 2016.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika mwaka 2018 idadi ya wanafunzi wanaotarajiwa kujiunga na kidato cha kwanza ni **4,891** (Wav **2,612,** Was **2,279**). Idadi hiyo ni kubwa zaidi kwa asilimia **74.8%** ukilinganisha na wanafunzi **1,236** waliomaliza kidato cha IV mwezi **Novemba, 2017.**

MATOKEO YA MITIHANI YA KITAIFA

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Hali ya matokeo ya mitihani ya Kitaifa katika shule za Sekondari Wilaya ya Serengeti kwa miaka mitatu ni kama ifuatavyo:- Mwaka 2016 ufaulu wa mtihani wa kidato cha **II** ulipanda kutoka **76%** mwaka 2015 hadi **89%** mwaka 2016 na kwa upande wa mtihani wa kidato cha **IV** ufaulu ulishuka kutoka 65.3**%** mwaka 2015 hadi **64.9%** mwaka 2016**.**

Hali ya mimba katika shule za Sekondari

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Uongozi wa Wilaya ya Serengeti unaendelea kupambana na changamoto ya tatizo la wanafunzi wa kike kupata ujauzito. Katika kipindi cha kuanzia Januari 2017 hadi Desemba 2017 jumla ya wanafunzi wa kike **27** wameripotiwa kupata ujauzito na wote waliondolewa shuleni. Kati ya wanafunzi hao waliopata ujauzito wanafunzi 11 kesi zao ziko mahakamani, 13 upelelezi wake unaendelea na 3 zimeshatolewa maamuzi kwa wahusika kuhukumiwa miaka 30 jela.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Changamoto iliyopo katika kukabiliana na tatizo la ujauzito kwa wanafunzi baadhi ya wanafunzi na wazazi/walezi kushindwa kutoa ushirikiano kwa uongozi wa shule, viongozi wa Kata na Jeshi la Polisi ili kuwachukulia hatua waliohusika kuwapa ujauzito wanafunzi.

Aidha, pamoja na juhudi hizo, Uongozi wa Wilaya umeweka mkakati wa kujenga Mabweni /Hosteli katika shule za Sekondari ili kukabiliana na tatizo la mimba ili kupandisha hali ya ufaulu kwa wanafunzi. Ujenzi wa mabweni unaendelea katika shule za Sekondari za Machochwe, Ngoreme na Robanda.

SEKTA YA MAJI

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya imeweza kutekeleza Miradi mbalimbali ya Maji ikiwa na lengo la kuhakikisha kuwa wananchi wanapata maji Safi na Salama. Hadi kufikia Desemba 2017, jumla ya watu 146,230.56 kati ya sawa na asilimia 58.68 ya watu wote waishio wilayani Serengeti wanapata maji safi na salama ukilinganisha na asilimia 42.80 ya watu 106,657.60 waliokuwa wanaopata maji safi na salama mwaka 2010.

Ujenzi wa Miradi ya Maji ya Vijiji

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP) Wilaya ya Serengeti inajenga miradi 11 na tayari imekamilisha miradi kwa gharama ya **Tsh 4,483,783,914.75** kwenye vijiji vya:-**Rung'abure, Mbalimbali, Masangura, Natta mbiso, Natta Motukeri, Kenyana/Nyamitita, Nyansurumunti, Nyagasense, Park nyigoti, Wegete na Kebanchabancha.**

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Ujenzi wa Miradi Maji ya Kenyana/Nyamitita na Kebanchabancha inayoendelea kujengwa/kukamilishwa, itagharimu Tsh.1,671,126,300. Miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali za ujenzi kama ifuatavyo:-Kenyana/Nyamitita 60% na Kebanchabancha 45%. Miradi yote inayotekelezwa itakapokamilika itatoa huduma kwa wananchi wapatao 156,231 sawa na asilimia 62.69 ya wananchi wote waishio vijijini.

Miundombinu ya Maji Vijijini

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilayaya Serengeti imeendelea kuboresha huduma ya maji katika maeneo mbalimbali vijijini kwa kuchimba visima na kujenga mitandao ya maji maeneo yaliyo na vyanzo vya maji. Shughuli za uboreshaji wa huduma za maji inafanyika kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali wa maendeleo ambao ni pamoja na Grumeti, Amref Health Africa kwa kushirikiana na Coca cola Africa Foundation na Usafi kwa Afya.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali kupitia mpango walipa kwa matokeo (PR) imetoa fedha kwa ajili ya kufufua vituo vya kuchotea maji 19 ambavyo havifanyi kazi ili kuweza kutoa huduma ya maji kwa wananchi kama ilivyokusudiwa katika vijiji 19 kukamilika kwa uboreshaji wa vituo vya kuchotea maji kutaongeza kiwango cha upatikanaji wa maji katika vijiji.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya ya Serengeti chini ya ufadhili wa CocaCola Africa kwa kushirikiana na AMREF Health Africa inatekeleza miradi ya maji kwenye vijiji vinne (4), Mradi huu ukikamilika utaongeza upatikanaji wa huduma ya maji kwa watu wapatao 7,000 sawa na asilimia 18.88 ya wakazi wote 37,067 wa kata nne (4) za Nyansurura, Kenyamonta, Mosongo na Busawe ambazo mradi utatekelezwa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilayaya Serengeti kupitia Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini ambayo itatekeleza miradi ya maji kwenye vijiji vya Kitunguruma, Busawe na Makundusi. Hadi sasa Wizara ya Maji na Umwagiliaji tayari imetuma fedha kwa ajili ya kufanya upimaji na usanifu wa miradi ambao umefanyika na Wizara imetoa kibali cha kutangaza zabuni kwa ajili ya ujenzi wa miradi hii.

Upatikanaji Maji katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mugumu

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Huduma ya maji katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mugumu imeimarika kwa mwaka 2017 ukilinganisha na 2015/2016 kwani mtandao wa mabomba umepanuka na kiwango cha maji kimeongezeka hadi kufikia 61% yawatu 46,932 wanaopata maji 2017ukilinganisha na 59% (2015).

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP) ukamilishaji wa ujenzi wa chujio Maji katika Bwawa la Manchira ili kuboresha ubora wa maji yanayotolewa katika eneo la Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mugumu unaendelea. Ujenzi huu wa chujio unasimamiwa na Mamlaka ya Maji Musoma (MUWASA).

Mradi wa ujenzi wa uwanja wa ndege.

Wilaya ina shabaha ya kufanya mji wa Mugumu kuwa kitovu cha utalii na lango la kuingilia Hifadhi ya Taifa ya Serengeti (SENAPA). Katika kufanikisha hili, kwa kushirikiana na wadau wengine wa maendeleo, hususani Grumeti Reserves Ltd, Wilaya ina mpango wa muda mrefu wa kujenga uwanja wa ndege ili kuwa kichocheo cha maendeleo katika eneo la kaskazini na kaskazini magharibi mwa mbuga ya Serengeti.

Uwanja huu wa ndege ukikamilika, Taifa litapunguza hasara kubwa ambayo inatokana na watalii wakubwa wanaoshindwa kutembelea mbuga ya Serengeti kwa sababu yakushindwa kutumia usafiri wa ndege Ndogo/ barabara .

Mradi huu unakadiriwa kugharimu kiasi cha Tshs. 15,000,000,000/= na hadi sasa kiasi cha Tshs. 1,257,488,799.00 zimetumika kwa mchanganuo ufuatao;

i. Fedha za fidia ya ardhi 400,000,000.00
ii. Kuhamisha shule ya Msingi ya Burunga 420,000,000.00
iii. Gharama za kutambua athari za mazingira (EAI) na usanifu 437,488,799.00

Fedha hizi zilitolewa na Grumeti Reserves Ltd.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, cheti cha tathmini ya athari za Mazingira na kibali cha ujenzi wa uwanja wa ndege vimeshatolewa. Utekelezaji wa mradi huu ulipangwa kutekelezwa kwa ubia na mwekezaji ambapo Halmashauri ilitarajiwa kuchangia Tshs. 5,000,000,000/= hadi sasa kiasi hicho cha fedha hazijapatikana. Hata hivyo bado tunayo nia ya kuwa na uwanja huo wa ndege wa Mugumu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mwisho tunaipongeza Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mhe. Dr. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhauri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada za kuinua uchumi wa nchi, kupiga vita rushwa na ufisadi, na kuleta nidhamu katika utendaji wa Serikali.

Naomba kuwasilisha.

Nurdin H. Babu
MKUU WA WILAYA
SERENGETI